**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI MBALATSE**
**MTIHANI WA ROBO MUHULA KIDATO CHA KWANZA**
**HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**

**MUDA: SAA 2:00** **MWEZI WA NNE 2025**

## MAELEKEZO:

1. Mtihani huu una jumla ya maswali **10** katika sehemu **A, B and C.**

2. Sehem **A** ina alama kumi na **tano (15),** sehemu **B** ina alama **sabini (70)** na sehemu **C** ina alama **kumi na tano (15)**

3. Jibu mwaswali yote katika sehemu zote.

4. Vitu visivyoruhusika haviruhusiwi katika chumba cha mtihani

5. Andika **jina kamili** katika kila ukurasa wa karatasi yako ya kujibia.

## SEHEMU A: (ALAMA 15)

**Jibu Maswali yote katika sehemu hii**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) – (v) kisha andika herufi ya jibu sahihi katika jedwali la kujibia.

(i). Benita ni Mwalimu wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili katika shule ya sekondari Magagula, alipoingia darasani kwa mara ya kwanza aliwaambia wanafunzi wake wapendwa kuwa somo la Historia ya Tanzania na Maadili linaundwa na dhana kuu mbili, nazo ni:
A. Mabadiliko ya Tanzania na Maadili yake
B. Historia ya Tanzania na Mabadiliko yake
C. Historia ya Tanzania na Maadili
D. Maadili na Historia ya Dunia

(ii). Kumekuwa na uhusiano mkubwa kati ya somo la Historia ya Tanzania na masomo mengine, ukiacha masomo mengine, somo hili lina husiana na somo la Jiografia kwa kuwa:
A. Somo la Jiografia linajihusisha kuelewa aina za vyakula walivyotumia babu zetu
B. Somo la Jiografia linajihusisha kutoa burudani kwa watu Tanzania
C. Somo la Jiografia linajihusisha kujua lugha mbalimbali walizotumia watu
D. Somo la Jiografia linajihusisha mazingira ambayo historia imetokea

(iii). Wahadimu ni jamii ya Wabantu wanaopatikana katika eneo la kati na kusini mwa kisiwa cha Unguja. Asili ya neno "hadimu" ni kiarabu lenye maana ya:
A. Kutoa huduma
B. Kuadimika
C. Wahudumu wa meli
D. Wahamiaji

(iv). Chimbuko la wabantu wa Tanzania ni?

A. Africa kusini
B. Africa magharibi
C. Africa mashariki
D. Africa kaskazini

(v). Kiongozi wa jadi wa jamii ya watumbatu alijulikana kwa jina la:
A. Mwanaheri
B. Mwana wa mwana
C. Mkama ndume
D. Mwinyi mkuu

(vi). Ili Taifa lolote liendelee watu wake hawana budi kushikamana na maadili, hivyo maadili yaweza kutafsiriwa kama ni:

A. Miongozo inayotawala tabia na matendo ya watu

B. Matendo yanayotawaliwa na watu mbalimbali

C. Miongozo inayotawala viongozi mbalimbali

D. Mambo muhimu yanayotawala historia ya watu

(vii). Nchi yetu ya Tanzania imeongozwa na Maraisi mbalimbali, wafuatao wametawala kwa kuongozana.

A. Nyerere kisha Mkapa

B. Mwinyi kisha Kikwete

C. Mkapa kisha Kikwete

D. Magufuli kisha Kikwete

(viii). Kiongozi mkuu katika jamii ya Washirazi aliitwa:

A. Mwana wa Mwana

B. Chifu

C. Nduna

D. Mwinyi Mkuu

(ix) Dhana au maana halisi ya Historia ya Tanzania ni:

A. Mfululizo wa matukio ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yaliyotokea nchini Tanzania.

B. Makabila ya Tanzania yalivyoendeleza utamaduni wao.

C. Maendeleo ya kiuchumi kutokana na kilimo na biashara za jadi hadi uchumi wa sasa.

D. Mkusanyiko wa familia kadhaa zenye uhusiano wa damu na asili moja.

(x) Kikundi kidogo cha watu wenye uhusiano wa damu au ndoa huitwa:

A. Familia

B. Taifa

C. Wakichembe

D. Wanilo

| (i). | (ii). | (iii). | (iv). | (v). | (vi). | (vii). | (viii). | (ix). | (x). |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Oanisha Makabila ambayo ni asili ya Tanzania yaliyo katika Kundi A na maelezo ya makabila hayo kutoka kundi B

| **ORODHA A** | **ORODHA B** |
|---|---|
| (i). Wabantu<br>(ii). Wakichembe<br>(iii). Wakushito<br>(iv). Wanilo<br>(v). Washirazi | A. Jamii ambayo ni wazawa halisi wa Tanzania<br>B. Jamii ambayo ni mchanganyiko wa Waafrika na Waasia iliyohamia kutoka kona ya bara la Afrika maeneo ya Somalia na Ethiopia<br>C. Jamii ya asili ya Tanzania iliyohamia kutoka kusini mwa Sudan<br>D. Jamii ya Wabantu iliyohamia na kuishi katika kisiwa cha Tumbatu<br>E. Jamii ya asili ya Tanzania iliyohamia kutoka nchi ya Naijeria na Kameruni.<br>F. Jamii ya asili ya Zanzibar iliyohamia kutoka ghuba ya uajemi iliyokuja kwa kutumia majahazi.<br>G. Jamii ya Wabantu iliyohamia na kuishi katika kisiwa cha Pemba<br>H. Jamii ya asili ya Tanzania iliyohamia kutoka nchi za Marekani na Uingereza |

| (i). | (ii). | (iii). | (iv). | (v). | (vi). |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

**SEHEMU B: (ALAMA 70)**

Jibu maswali yote kwenye sehemu hii

2. Taja masomo walau matano yanayohusiana na somo la Historia ya Tanzania na maadili.
   (i). ………………………………………………………………………………
   (ii). ………………………………………………………………………………
   (iii). ………………………………………………………………………………
   (iv). ………………………………………………………………………………

(v). ………………………………………………………………………………………

4. (a) Nini maana ya urithi?

……………………………………………………………………………………...................
……………………………………………………………………………………...................

(b) Wazee ambao ni watangulizi wetu katika Taifa la Tanzania wametuachia urithi ambao mpaka leo tunajivunia nao. Taja aina kuu tatu za urithi wa Tanzania:

(i) ……………………………………………………………………………….......

(ii) ………………………………………………………………………………......

(iii) ……………………………………………………………………………….....

5. Tunu ni jambo ambalo watu hupewa bila kuomba, Tanzania imebarikiwa tunu mbalimbali. Taja tunu tano za taifa la Tanzania:

(i)
………………………………………………………………………………………

(ii) ………………………………………………………………………………………..

(iii) ……………………………………………………………………………………….

(iv) ………………………………………………………………………………………

(v) ……………………………………………………………………………………....

6. (a). Nini maana ya Kabila?…………………………………………………………

……………………………………………………………………………………….......
............

(b). Taja makabila manne (4) ya jamii ya Wabantu.

(i). ……………………………….................................................................................

(ii). ……………………………….................................................................................

(iii). …………………..……………..............................................................................

(iv). ……………………………….................................................................................

7. (a). Eleza maana ya jamii
…………………………………………………………………………...........

………………………………………………………………………………………...
.................

(b). Taja makundi **matatu (3)** yanayounda Jamii

(i). ………………………………………………………............................................

(ii). ………………………………………………………............................................

(iii). ………………………………………………………............................................

8. Serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania haikuanzisha ufundishwaji wa somo hili la Historia ya Tanzania na Maadili kwa kukurupuka, bali ilizingatia faida zinazopatikana. Kwa kifupi fafanua faida tano (5) za somo la Historia ya Tanzania na Maadili.

(i). ……………………………….........................................................................

(ii). ………………………………………………….................................................

(iii) ………………………………………………….................................................

(iv). ……………………………………………………………………………………………

(v). ………………………………………………………………………………………

(vi). ………………………………………………………………………………………

9. Orodhesha matendo **matano (5)** ambayo ni ya kimaadili katika jamii.

(i). …………………………………………………………………………………………….

(ii). …………………………………………………………………………………………….

(iii). …………………………………………………………………………………………….

(iv). …………………………………………………………………………………………….

**(v).** …………………………………………………………………………………………….

**SEHEMU C: (ALAMA 15)**

Jibu swali la kumi (10)

10. Jamii ya Wabantu ni miongoni mwa jamii za kale zilizosambaa maeneo mengi barani Afrika. Kwa mifano halisi eleza sababu sita (6) zilizosababisha makundi makuu ya jamii za asili za Tanzania kuhama na kusambaa maeneo mbalimbali.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..........
.........................................